

Mambo yahusianayo na afya



Mycobacterium Avium Complex (MAC)

MAC Ni Nini?

- MAC ni kifupi cha Mycobacterium avium complex. Ni kijimea kinachofanana na vijidudu vinavyoambukiza kifua kikuu (TB). Hata hivyo, MAC huwa haambukizwi kama kifua kikuu kinavyoambukizwa. Kifua kikuu kinaweza ambukizwa kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa kukaribiana na kukohoa, ila MAC huambukizwa kwa njia nyingine tofauti.

Je, Mtu Huwezaje Kuambukizwa MAC?

- Kijidudu cha MAC hupatikana kwenye udongo na maji. Watu wengi wanaweza kuwa wameshakutana nacho. Bali kwa watu wenye mfumo wa kupigana na magonjwa ulio na afya na ufanisi nzuri, kijidudu hiki mara nyingi hakiwezi sababisha ugonjwa. Kwa watu wenye maambukizi ya vijidudu vya ukimwi ambao vipimo vyao vya CD4 vipo chini ya 100, MAC huweza sababisha ugonjwa wa hatari sana.

Je, Dalili Za MAC Ni Zipi?

- Dalili za MAC huweza kujionyesha na kuambatana na homa, baridi, kupunguwa kwa uzito wa mwili, kutokwa jasho usiku, uharo wa maji maji, maumivu ya tumbo, udhahifu na kuchoka kila mara. Huweza pia sababisha upungufu wa damu mwili (kupunguwa kwa chembe nyekundu za damu mwilini mwako).



Canadian AIDS Treatment
Information Exchange
Réseau canadien
d'info-traitements sida

www.catie.ca



www.apaa.ca

Maamuzi juu ya matibabu ya aina mbalimbali yanahitajika kufanywa kwa kushauriana na mtaalamu aliyehitimu kwenye mambo ya afya na mwenye ujuzi juu ya magonjwa yanayoendana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi na matibabu atakayoamuliwa kutumiwa.

Mycobacterium Avium Complex

- MAC ni kijimea kinachuwa polepole, hivyo dalili zake huweza kuonekana kwa mbali mwanzoni ila kuendelea kuwa mbaya wiki na miezi inavyopita.
- MAC huweza gunduliwa kwa kipimo cha damu. Kama kipimo chako cha CD4 kipo chini ya 100, daktari wako atahitajika kuchukuwa kipimo cha damu kinachoweza kuchunguza na kupima kama una maambukizi ya MAC.

Je, Ni MAC Huweza Kuzuiliwa vije?

- Kwa kuwa MAC husababisha ugonjwa kwa watu wenye mfumo dhaifu wa kupigana na magonjwa (kipimo cha CD4 chini ya 100), njia nzuri ya kuzuia MAC ni kuwa na afya bora na kuhakikisha kuwa kiwango chako cha chembechembe za CD4 kinakuwa kipo juu.
- Dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi zinaweza kukusaidia kuimarisha mfumo wako wa kupigana na magonjwa na kuweka kiwango chako cha CD4 juu.
- Kama kipimo chako cha CD4 kipo chini ya 100, unaweza kutumia baadhi ya dawa kuzuia MAC. Katika dawa zinazotumika kuzuia MAC ni kama:
 - azithromycin (Zithromax) miligramu 1,200 mara moja kwa wiki kwa kumeza kidonge hiki
 - Clarithromycin (Biaxin) miligramu 500 mara mbili kwa ziku kwa kumeza kidonge hiki
 - Rifabutin (Mycobutin) miligramu 300 mara moja kwa siku kwa kumeza kidonge hiki

Je, MAC Huweza kutibiwa vije?

- MAC ni kijidudu kigumu kutibiwa na huweza kuwa sugu na nguvu ya dawa moja, hivyo mchanganyiko wa dawa kadhaa kwa pamoja huhitajika kama una MAC.
- Dawa zinazojulikana na ambazo zinaweza tumika kwa pamoja kutibia MAC ni kama:
 - clarithromycin (Biaxin)



Mycobacterium Avium Complex

- azithromycin (Zithromax)
 - rifabutin (Mycobutin)
 - ciprofloxacin (Cipro)
 - ethambutol (Myambutol)
- Uchaguzi wa dawa gani unaweza kutumia utategemea pia afya yako kwa ujumla, dalili zako, dawa gani zinaweza kukuletea madhara kadhaa ukizitumia, na dawa nyingine za maambukizi ya vijidudu vya ukimwi unazotumia n.k.
 - Dawa hizi utakazotumia hazitaweza kukiua kijimea chote MAC, kwa hiyo matibabu haya mara nyingi huhitajika kuendela kwa maisha yako yote.
 - Kutokana na tafiti na gunduzi za kisanyansi zinazoendelea hivi sasa katika kutafuta tiba ya maambukizi ya vijidudu vya ukimwi, watu wengi wamepa nafuu na maendeleo mazuri katika viwango vya vipimo vyao vya CD4. Kiwango chako cha CD4 kikipanda zaidi ya 100 na kuendelea kuwa juu ya 100 kwa miezi kadhaa, unaweza kusitisha matibabu ya MAC. Ongea na daktari wako juu ya uwezekano huu.

Shirika la kubadilishana maelezo juu matibabu ya ukimwi Kanada (The Canadian AIDS Treatment Information Exchange – CATIE) na Shirikisho la waafrika katika kupigana na ukimwi (Africans in Partnership Against AIDS - APAA) kwa nia nzuri kabisa wanatoa maelezo kwa watu wanaoishi na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi/Ukimwi ambao wangependa kutawala afya zao wenyewe kwa kushirikiana na wataalamu wa afya wanaowapatia matibabu. Hata hivyo, maelezo haya yanayochapishwa au kutolewa na CATIE au APAA hayawezi kuchukuliwa kama ushauri wa kiafya. Hatushauri au kusisitiza juu ya tiba moja juu ya nyingine. Hivyo tunawashauri watumiaji ya maelezo yetu kupitia maelezo ya matibabu mengine yanayotolewa na vyanzo mbalimbali kwa upeo mkubwa iwezekanavyo. Tunawashauri watumiaji wa maelezo haya na kusisitiza kuwa ni muhimu kushauriana na wataalamu wa afya na tiba waliohitimu mafunzo yao kabla ya kuamua, kutumia au kuanza jambo lolote juu ya matibabu.

Vile vile, hatuthibitishi au kudhamini ukweli au ufarisi na ujuzi wa maelezo yanayochapishwa au kupatikana kutoka CATIE au APAA. Watumiaji wanaotumia au kutegemea maelezo haya wanafanya hivyo kwa kuthubutu wenyewe na matokeo yake yakiwa mabaya yatakuwa juu yao. Si CATIE wala APAA, au Wizara ya Afya Kanada, au wafanyakazi wao, wakurugenzi, maafisa au watu wanaojitolea wataweza kuhusishwa na uharibifu wa aina yeyote unaoweza kutokea kwa kutumia vizuri au vibaya maelezo haya. Mawazo na maelezo yaliyotolewa hapa au kwenye nakala yeyote au ilani/tangazo lolote.

Copyright: This Fact Sheet is made available through a collaboration between Africans in Partnership Against AIDS (APAA), Asian Community AIDS Services (ACAS) and the Canadian AIDS Treatment Information Exchange (CATIE). Original content developed by ACAS, 2001. Translation into Swahili and Hausa by APAA, 2004.

This information is also available in Chinese, Tagalog and Vietnamese

Funding has been provided by Health Canada, under the Canadian Strategy on HIV/AIDS

Supported by an unrestricted educational grant from GlaxoSmithKline in partnership with Shire BioChem



partnership
in partnership with

